RASIMU YA HOTUBA YA MGENI RASMI, MHESHIMIWA JOB YUSTINO NDUGAI, SPIKA WA BUNGE LA JAMHURI YA TANZANIA, ILIYOSOMWA KWA NIABA YAKE NA MH. AZAM ZUNGU, MWENYEKITI WA BUNGE LA JAMHURI YA TANZANIA NA MBUNGE WA ILALA, KWENYE SHEREHE ZA KUADHIMISHA MIAKA 17 YA SHULE NA MAHAFALI YA 15 YA WANAFUNZI WA KIDATO CHA NNE YA SHULE YA SEKONDARI YA WASICHANA YA BARBRO JOHANSSON;
JUMATATU TAREHE 25 SEPTEMBA 2017, LUGURUNI, DAR ES SALAAM

Mheshimiwa Mwenyekiti Mwanzilishi wa Joha Trust Professa Anna Kajumulo Tibaijuka, Mbunge Muleba Kusini;

Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya Barbro Johansson, Bwana Salmon Odunga, wajumbe wa bodi na waanzilishi;

Balozi wa Sweden nchini Tanzania, Mheshimiwa Katrina Ragnitt;

Afisa Elimu Mkoa wa Dar es Salaam, Bwana Hamisi Lissu, Afisa Elimu wa Manispaa ya Ubungo Bibi Neema Maghembe na viongozi wa Serikali mliopo katika hafla hii;

Viongozi wa Mtaa wa Kwembe;

Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi na Walimu (PTA), Dr. John Kyaruzi na Kamati nzima ya PTA ya sasa na zilizotangulia;

Mkuu wa Shule Barbro Johansson Bibi Halima Kamote,

Wakuu wa Shule, Walimu na Wanafunzi kutoka Shule za Sekondari jirani na zile za Mradi wa majaribio wa kuboresha elimu kwa mtoto wa kike;

Wahitimu wa Kidato cha IV na wanajumuia wa Shule ya Barbro Johansson;

Wazazi na Wageni waalikwa;

Waandishi wa habari;

Mabibi na Mabwana.

Awali ya yote napenda kutoa shukrani zangu kwako Mwenyekiti wa Bodi ya Udhamini, Mwenyekiti Mwanzilishi wa Barbro Johansson, Mkuu wa Shule na uongozi mzima wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Barbro Johansson

(Shule ya Barbro) kwa mwaliko wenu kwangu kwenye Sherehe hizi za kuadhimisha miak 17 tangu kuanzishwa kwa Shule hii na mahafali ya 15 ya Kidato cha Nne. Ni furaha kwangu kujumuika nanyi kushuhudia matunda ya kazi ngumu mliyoifanya ya kuelimisha wanafunzi, hasa wa kike katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kupanua utoaji wa elimu ya sekondari nchini.

Aidha, napenda kutumia fursa hii kukupongezaMheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na wajumbe wa Bodi yako, Mkuu wa Shule, walimu na wafanyakazi wote wa Shule ya Barbro kwa kuiongoza vema Shule hii kwa miaka 17 sasa. Ni matumaini yangu kwamba mtaendelea kusimamia vizuri utoaji wa elimu na uendeshaji wa shule hii kwa ufanisi zaidi, hasa kwa kuzingatia mabadiliko ya kiuchumi na ya kijamii yanayoikabili nchi yetu hivi sasa.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,
Baada ya kusikiliza taarifa fupi ya historia ya Shule na maelezo juu ya maendeleo yake, nimebaini kwamba Shule hii imepiga hatua kubwa tangu ianzishwe mwaka 2000. Nimeambiwa kwamba, tangu Shule ianzishwe, takriban wasichana wa Kitanzania 2080 wamekwishafaidika na kuhitimu elimu yao ya sekondari, yaani Kidato cha 4 na cha 6 na kwamba asilimia 99.9 ya wanafunzi hawa walifaulu na kuendelea na masomo katika ngazi za juu. Aidha, nimeelezwa kuwa Shule hii inang'ara kitaaluma na mwaka jana wanafunzi wote wa kidato cha pili, cha nne na cha sita walifaulu katika mitihani yao ya taifa. Ufaulu katika masomo na katika nyanja nyinginezo ni ishara tosha kuwa wasichana wakipewa nafasi wanaweza, hata katika masomo ya sayansi yanayodhaniwa kimakosa kuwa ni magumu. Napenda kutumia fursa hii kuwapongeza sana walimu, wanafunzi na wafanyakazi wote kwa kufanya kazi kwa bidii, ufanisi na uvumilivu hadi kufikia mafanikio haya. Tafadhali endeleeni kukaza uzi katika utendaji wenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti,

Nimefurahishwa na mazingira ya shule na nimefahamishwa kuwa asilimia 90 ya miti iliyopo ndani ya shule mmeipanda nyie wanafunzi wenyewe. Elimu hii ya kutunza mazingira na upandaji wa miti muipeleke kote muendako ili kuifanya dunia yetu iwe mahali pazuri pa kuishi na tuweze kuacha urithi wa mazingira bora kwa watoto wetu na vizazi vijavyo.

Mabibi na mabwana,
Kama mjuavyo,Sekta ya Elimu Tanzania ina nia ya kutoa elimu bora kwa wanafunzi wengi zaidi, lakini mara nyingi katika mipango kama hii, upungufu wa bajeti umekuwa kikwazo kikuu. Ushirikiano kati ya Serikali na Sekta Binafsi kama Joha Trust utaongeza ufanisi katika kutimiza azma hii.

Ninawapongeza sana kwa mradi wa majaribio wa kueneza mambo mema ya Shule ya Barbro kwenye shule jirani. Kama shule mfano kuna mengi ya kuigwa hivyo niwashukuru kwa kutokuwa wachoyo wa mambo yaliyowasaidia kutoa elimu bora. Nimetaarifiwa kwamba nguzo kuu za mradi huu ni 5 yaani nidhamu bila kiboko, ushirikiano wa walimu na wazazi kupitia umoja wa wazazi na walimu, ushauri nasaha, klabu za wanafunzi na msaada wa ziada wa kitaaluma kwa wanafunzi wenye ufaulu wa chini. Kama ambavyo Mkuu wa Shule ameeleza kuwa tayari matokeo ya awali chanya yameonekana, naamini mradi huu utabadilisha kiwango cha elimu katika shule husika na hatimaye mbinu hizi kusambaa kwenye shule nyingi zaidi nchini.

Wageni waalikwa, mabibi na mabwana,

Mkuu wa Shule ameongelea juu ya changamoto nyingi mnazokabiliana nazo na kuu ni juu ya upatikanaji wa fedha za kufadhili wasichana wenye uwezo mkubwa kitaaluma lakini wanaotoka kwenye familia zenye kipato duni. Naamini taasisi, asasi za kijamii na watu wote wenye uchungu na elimu watasaidia katika kuchangia juhudi za kufadhili wasichana wenye sifa kwenye Shule hii ya Barbro. Hili ni jukumu letu sote kama jamii, kwani watoto hawa pia ni sehemu ya jamii na wanayo haki ya kupata elimu bora kwa kuwa kikwazo kwao si ufinyu wa maarifa, bali ni hali ngumu kiuchumi ya familia zao.

Ninachukua nafasi hii kutoa shukrani kwa Serikali ya Sweden na marafiki wa shule hii wa Sweden ambao wameendelea kutoa msaada wa kuwasomesha wasichana hao wahitaji katika shule hii. Baada ya kuelezwa changamoto zilizopo, upo umuhimu wa sisi wanajamii na viongozi wengine wa shule kuhamasisha na kutafuta misaada ili lengo la Shirika hili la Elimu la kuwafadhili watoto wahitaji wenye vipaji kusoma katika shule bora liendelee. Kwa sisi ambao tumebahatika kupata elimu na kupewa nafasi za uongozi, jambo hili tulione kuwa ni changamoto na kutafuta ufumbuzi wa kina.

Wapendwa wahitimu,
Ni vema mkafahamu kwamba ulimwengu wa sasa unahitaji wasomi wenye upeo wa juu kuelewa mambo na kutatua matatizo. Jambo ambalo ningependa muendelee kulizingatia kwa makini ni kwamba elimu mliyoipata bado ni mwanzo tu, hasa ukizingatia kukua kwa utandawazi (globalization). Siku hizi mabadiliko ni ya haraka haraka mno na yanagusa kila mtu na kila nyanja ya maisha. Ni vizuri mkajua kwamba ni wajibu wenu kuendelea kujifunza mbinu mpya za kuyakabili mabadiliko haya. Kama Mkuu wenu wa Shule alivyosema ninatarajia kuwa ninyi nyote mliohitimu Kidato cha 4 leo mtaendelea na elimu ya juu sekondari ya kidato cha tano na sita na hatimaye vyuo vikuu kulijengea taifa hazina bora ya rasilimali watu iliyoelimika.

Mkumbuke kuwa elimu yenu nzuri mliyopata na ambayo mtaendelea kuipata itafungua maisha yenu na ya jamii nzima ikiwa ni pamoja na familia zenu na watoto wenu. Elimu hii pia itawapa uwezo wa kiuchumi, itawapa uwezo wa kuwa na sauti, mtaongea na mtasikika na kusikilizwa, pia itawajengea heshima katika jamii na kuwapa uwezo wa kuchagua mambo mbali mbali katika maisha. Mifano hai tunayo na mmojawapo ni ule ambao wote mnaujua na mnao hapa hata leo. Nafasi ya Mwenyekiti wenu Mwanzilishi Mhe. Prof. Anna Tibaijuka, MB. ni mfano wa kuigwa na napenda uwe hamasa kwenu katika kujiwekea malengo kielimu, katika kutumikia jamii na kimaisha. Nawaasa tuangalie mifano iliyopo na tujifunze. Ninawapongeza na wazazi wenu ambao wamejitoa kulipa karo ili mpate nafasi kulelewa katika mikono ya watu wenye uzoefu wa hali ya juu. Wasichana ninawaasa muwaenzi sana wazazi wenu kwa kusoma kwa bidii hata huko muendako. Mmepata fursa adimu basi tukayaone matunda yake.

Ndugu Wageni Waalikwa, Mabibi na Mabwana,
Ningependa kuwakumbusha wahitimu mambo mengine mawili muhimu sana. Nayo ni kuhusu kuwa waadilifu maishani pamoja na kuwa wajasiriamali. Naamini kwamba wakati wa maisha yenu hapa shuleni walimu wenu wamekuwa wakisisitiza kuwa mfuate taratibu na sheria za shule. Mjue kwamba hilo linafanyika kuhakikisha kwamba katika siku za baadae nyote mnakuwa waadilifu katika kila mnalotenda maishani mwenu. Pia, napenda kuwasisitizia juu ya umuhimu wa elimu ya ujasiriamali. Siku hizi ajira za maofisini ni haba, lakini fursa za kujiinua kiuchumi zipo tele nchini kwetu. Vijana hamna budi kuziibua fursa zilizopo na kuzifanyia kazi ili muweze kujiajiri na kuwaajiri wenzenu. Nimefurahi sana nilipoambiwa ya kwamba hapa shuleni kuna klabu mbalimbali ikiwemo ya wajasiriamali ambayo naamini inafanya kazi nzuri ya kuwafungua macho kuwa ajira binafsi kupitia ujasiriamali zinalipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wageni waalikwa, mabibi na mabwana,
Haya ni mahafali na nisingependa kuwachosha na hotuba ndefu. Nawapongeza tena wote walioshiriki kufanikisha mahafali yetu ya leo. Ningependa niwashukuru sana wafadhili wote wa Shule ya Barbro wakiwemo Serikali ya Tanzania, Serikali ya Sweden kupitia Ubalozi wake nchini, Joha Trust Sweden, Wazazi wa Shule ya Barbro kupitia umoja wao wa PTA na wengine wote ambao michango yao imeifikisha shule hii na wanafunzi wetu hapa walipo. Nawaomba waendelee na moyo huo na wengine zaidi tujiunge. Kuchukua majukumu kwenye jamii ni ishara njema na hivyo sote tushirikiane kuhamasisha misaada ya kwa ajili ya wahitaji.

Nimalizie kwa kuwapongeza tena Wahitimu wetu. Mmefanya kazi nzuri **Hongereni sana**! . Binti yangu Gloria Ndugai ni mmoja kati ya wahitimu leo na sina budi kuwashukuru walimu kwa kazi nzuri mliyofanya kuwaandaa wanafunzi hawa hadi leo tunaposhuhudia kuhitimu kwao. Nawapongeza na kuwashukuru wazazi wenzangu na walezi wote kwa kujinyima ili kuhakikisha tunawapatia watoto wetu elimu bora. **Hongera sana kwetu kwa kutimiza wajibu wetu wa msingi.**

Mwisho, niwashukuru tena Bodi ya Shule kwa kunialika nishiriki nanyi kama mgeni wenu rasmi katika Mahafali hii. Hakika ukimuelimisha mwanamke umelielimisha taifa zima.

Nawatakia wote maisha mema na Mwenyezi Mungu awazidishie neema zake na Baraka, tupate mafanikio.

Asanteni kwa kunisikiliza.